


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA



13/06/2022

TANGAZO LA ZABUNI
NAMBA YA ZABUNI LGA/022/2021-2022/HQ/W/01

ZABUNI YA MAFUNDI (LOCAL FUNDI) KAZI YA UJENZI WA MSINGI WA JENGO LA
UTAWALA LA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

1. Halmashauri ya wilaya ya Kongwa imetenga fedha za Ujenzi wa JENGO LA UTAWALA LA HALMASHAURI ya Wilaya ya Kongwa mwaka wa fedha 2021/2022.
2. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa anakaribisha maombi ya kazi ya Ufundi kutoka kwa mafundi wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi za Ujenzi wa Msingi JENGO LA UTAWALA LA HALMASHAURI ya Wilaya ya Kongwa kwa kazi zifuatazo:-

NA	AINA YA ZABUNI	NAMBA YA ZABUNI
1.	Ujenzi wa Msingi wa JENGO LA UTAWALA LA HALMASHAURI ya Wilaya ya Kongwa	LGA/022/2021-2022/HQ/W/01

Sifa za mwombaji:-

- Muombaji awe ni Fundi mwenye uzoefu wa miaka isiyopungua mitano na aonyeshe uzoefu katika ujenzi.
- Muombaji awe ni mtanzania mwenye akili timamu na awe na umri wa

miaka kumi na nane na kuendelea (Aambatanishe kitambulisho cha utaifa - NIDA)

- Muombaji katika maombi yake achanganue kazi hatua kwa hatua kama ili vyoainishwa na kuonesha gharama za kila hatua ya kazi zilizomo kwenye kabrasha.
- Muombaji awe na uzoefu wa kujenga majengo ya serikali na mwenye uangalizi mzuri wa mali wakati wa utekelezaji wa mradi (Kuambatanisha uzoefu huo)
- Muombaji ajue vema kusoma ramani na vipimo vyake kwa ajili ya ufanisi wa kazi
- Muombaji aonyeshe muda wa utekelezaji wa mradi.
- Muombaji awe na akaunti ya benki iliyo hai yenye jina sawa na analoombea kazi
- Muombaji awe na cheti cha Ufundi sanifu FTC na kuendelea. (kuambatanisha vyeti)
- Muombaji aambatanishe wasifu wake pamoja na uzoefu wa kazi hizo ndani ya wasifu.
- Muombaji lazima awe na mafundi wasaidizi na vibarua wakutosha
- Fundi awe eneo la kazi muda wote wa kazi na awe tayari kufanya kazi siku zote za wiki.

3. Waombaji wanaweza kupata taarifa/ufafanuzi zaidi kuhusu kazi hizo katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi/Mhandisi wa Ujenzi wa Wilaya saa 2:00 Asubuhi Hadi saa 9:30 Alasiri siku za kazi (**Jumatatu hadi Ijumaa**).

4. Maombi yafungwe kwenye bahasha ya kaki yenye lakiri. Juu ya bahasha ionyeshwe aina ya zabuni na namba ya zabuni. Zabuni zitumwe kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni kwa anuani ifuatavyo:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmasauri ya Wilaya,
S.L.P 57,
Kongwa.**

5. Maombi ya zabuni zote yawasilishwe katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Mwisho wa kupokea maombi hayo ni **Jumane, 21/06/2022, saa nne kamili (4:00) Asubuhi**. Waombaji au wawakilishi wao, wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo utakaofanyika

Jumane, 21/06/2022, kuanzia saa nne kamili (4:00) Asubuhi katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi.



.....

Dr OMARY NKULLO

MKURUGENZI MTENDAJI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

MKURUGENZI MTENDAJI

HALMASHAURI YA WILAYA

S.L.P 57

KONGWA